

TANGAZO

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA




16/07/2018

MDC.H/.10/3/51

**MKURUGENZI MTENDAJI WA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA
ANAPENDA KUWATAARIFU WANANCHI
WOTE NA WAMILIKI WA VYOMBO VYOTE
VYA USAFIRI WA ABIRIA KUANZIA TAREHE
01/08/2018 VYOMBO VYOTE VYA USAFIRI
VITAANZA KUTUMIA STENDI RASMI YA
HALMASHAURI ILIYOPO ENEO LA MNADA
NDUGUTI.**

**PIA WANANCHI WANAOHITAJI KUPATA
VIBANDA VYA BIASHARA KWENYE ENEO LA
STENDI WAFIKE OFISI YA MKURUGENZI
MTENDAJI IDARA YA ARDHI.**

**NAWATAKIA UTEKELEZAJI MWEMA KATIKA
MAENDELEO YA HALMASHAURI YETU**


Eng. Godfrey T. Sanga

Mkurugenzi Mtendaji (W)

MKALAMA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Email: ded.mkalamadc@singida.go.tz

Simu Na. 026-2964000
Kwa kujibu, taja



Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
P. O. Box. 1007,
MKALAMA

Kumb. Na. MDC/H.10/3/51

16/07/2018

TANGAZO LA KAZI YA MUDA YA KUKUSANYA USHURU WA HALMASHAURI.

Mkurugenzi Mtendaji (W) anawatangazia wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama kuomba nafasi za kazi ya muda (yaani kibarua) ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri unaotokana na vyanzo vya ndani, Ajira hii itakuwa ni ya mkataba wa miezi mitatu ambao unaweza kuhuishwa kulingana na umahiri na utendaji kazi wa mtumishi.

1.0. SIFA ZA MWOMBAJI

- 1.1. Mtanzania ye yeyote aliyemaliza darasa la saba, anayejua kusoma na kuandika
- 1.2. Awe Raia wa Tanzania
- 1.3. Awe na umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka arobaini na tano (45)
- 1.4. Awe ana afya njema
- 1.5. Awe na wadhamini wawili, wenye makazi na mali zisizohamishika ndani ya Wilaya ya Mkalama
- 1.6. Asiwe amewahi kuhukumiwa na Mahakama ye yeyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kosa la Jinai

2. KAZI ZA KUFANYA

- 1.1 Kupokea fedha za ushuru wa mapato ya ndani
- 1.2 Kutoa stakabadhi kwa kutumia mashine za kieletroniki

- 1.3 Kuwasilisha fedha za makusanyo kila siku kwa Mweka Hazina wa Wilaya.
- 1.4 Kazi nyingine utakazopangiwa na Mkurugenzi Mtendaji

UJIRA


Ujira utakuwa wa ni **Tsh. 200,000** kwa mwezi na posho ya chakula ya **Tsh. 60,000** kila mwezi.

2. MAELEZO KWA UJUMLA

- (a) Barua zote za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Taaluma, Elimu na cheti cha kuzaliwa, pamoja na picha moja ya rangi (*passportsize*) ya hivi karibuni
- (b) Maombi yote yaambatanishwe na barua ya utambulisho kutoka Serikali ya kijiji/Mtaa ambao mwombaji anaishi.
- (c) Kila mwombaji aandike kwa usahihi anwani yake na namba yake ya simu inayopatikana muda wote kwa ajili ya mawasiliano
- (d) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **27/07/2018** Saa **9.30**
Alasiri
- (e) Waombaji watakaoitwa kwenye mchujo wa awali ndio wataitwa kwenye usaili
- (f) Masharti mengine ya kazi yataainishwa kwenye Mkataba wa kazi
- (g) Maombi yote yatumwe kwa

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S. L. P 1007
MKALAMA.

Au yawasilishwe ofisi ya Masijala wazi iliyopo jengo kuu la Halmashauri
ya Wilaya ya Mkalama Nduguti
Imetolewa na,


Eng. Godfrey T. Sanga
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MKALAMA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA